

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI MAKUNGU,
S.L.P 30,
MGOLOLO,
15.12.2020.

KUMB.NA.MAKSS/VOL

NDG.....

.....

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKUNGU WILAYA YA
MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 na unatakiwa kuripoti tarehe 11.01.2021 jumatatu saa 1:00 asubuhi. Shule ya sekondari Makungu ipo wilaya Mufindi, tarafa ya Kasanga, kata ya Makungu, katika kijiji cha Lugolofu.

Shule ni ya kutwa na ni ya mchanganyiko wa wanafunzi wavulana na wasichana, kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne. Huduma ya hostel inatolewa kwa wanafunzi wa jinsia zote wanaohitaji. Masomo yanayofundishwa ni Uraia, Kiswahili, Kiingereza, historia, jiografia, fizikia, kemia, baiolojia, hisabati. Somo la Literature in English hufundishwa kuanzia kidato cha tatu kwa wanafunzi wanaohitaji.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1.WAVULANA.

- Suruali(1)moja ya rangi ya **damu ya mzee** isiwe na muundo wa jinsi. Iwe na selebrasheni mbili.
- Suruali (1)moja ya **rangi ya kijivu** iliyokolea(dark grey)
- Mashati meupe mawili mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili. Viatu viwe vyenye kamba visiwe na kisigino kirefu.viwe vya kungarishwa na kiwi
- Tai moja rangi damu ya mzee moja.
- Tai moja rangi ya kijivu iliyoiva(dark grey)
- Soksi nyeusi jozi mbili.
- Sweta moja rangi damu ya mzee lenye umbo la 'V' kifuani.
- Sweta moja dark blue lenye umbo la V kifuani
- Bukta na fulana za michezo.
- Raba za michezo.
- Mkanda mweusi.

➤ **WASICHANA.**

- Sketi mbili.moja ya damu ya mzee(maroon)yenye mshono wa marinda kumi na mbili na ya pili ni rangi ya kijivu iliyokolea(dark grey) yenye mshono wa linda box pana yenye pindo mbili pembeni.
- Mashati meupe mawili mikono mirefu.
- Tai mbili .moja rangi damu ya mzee na nyingine iwe rangi ya kijivu iliyokolea(dark grey)
- Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na kisigino kirefu.viwe vya kufunga na kamba
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Sweta 2.moja rangi damu ya mzee lenye umbo la 'V' kifuani na nyingine dark blue.
- Track na fulana za michezo
Kwa watakaovaa hijabu ni lazima rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule.mfano nyeupe.

MAHITAJI MENGINE YA SHULE.

- ❖ Madaftari 20, kumi **counter book** ya masomo ya darasani na kumi **daftari za kawaida** kwaajili ya mazoezi na majaribio ya kila wiki. Kila somo litakuwa na daftari lake maalumu la mazoezi na majaribio.
- ❖ Begi (hand bag) ndogo jeusi kwa ajili ya kuwekea daftari na vifaa vingine vya masomo
- ❖ Kamusi (Dictionary) ya kiingereza – kiswahili au kiingereza- kingereza
- ❖ Mkebe wa hesabu mmoja (mathematical set 1)

NB. Ukaguzi wa sare na vifaa utafanyika ili kuhakikisha kila mwanafunzi ana sare na vifaa alivyoagizwa.

03.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HIL.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana na elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi katika Appendix A, B na C.

KARIBU SANA MAKUNGU SEKONDARI

.....
MDALINGWA, F.J
MKUU WA SHULE.

SHULE YA SEKONDARI MAKUNGU
S.L.P 30 MGOLOLO - IRINGA

APPENDIX C

DAKTARI

HOSPITALI YA

S.L.P

FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI.

Tafadhali tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake, na uthibitisha kama ataweza kumudu masomo ya sekondari shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa.

.....
MDALINGWA, F.J
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MAKUNGU,
S.L.P 30,
MGOLOLO.

YAH: MWANAFUNZI

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Urine
2. Stool
3. BP
4. Pregnancy test
5. Spleen
6. Chest
7. Physical abnormality

Nathibitisha kuwa mwanafunzi huyu ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari kwa sababu

JINA LA DAKTARI

SAHIHI/CHEO

TAREHE

.....

.....

.....